FADEMO SOCIAL PROTECTION FUND

MAAZIMIO YA MKUTANO MKUU WA SEPTEMBA 2027

HOTELI YA BARTH APARTMENTS, UHINDINI DODOMA.

JUMAMOSI YA 19.09.2026

Mambo Makuu yaliyojadiliwa Dodoma 2026

1. Taarifa ya Mapato na Matumizi ya Mfuko kuanzia Januari hadi Sept 2026 ambayo ilionesha Mfuko kukua sana kifedha kuanzia Januari 2026.
2. Saikolojia ya Kwa nini watu wengi Hushindwa kuwekeza na kwa nini wakishaumizwa kwa kupoteza fedha wanakata tamaa ya kuwekeza.
3. Matukio yaliyotokea mwaka 2026, watu Zaidi ya 913 waliopewa elimu ya fedha mikoa na wilaya Mbalimbali na Mafanikio makubwa yaliyopatikana
4. Mada ya Mfumo wa **Fademo App** na **Web System** na Matumizi yake, changamoto zake na hali ya usalama wa mifumo ya Fademo.
5. Mafao na Uwekezaji, fursa ya kuwa Balozi wa Fademo na fursa ya kuuza Vitabu na kupata kipato cha ziada. Kila mmoja anakaribishwa.
6. Usalama wa Mifumo ya Mfuko wa FADEMO. Uongozi wa FADEMO uhakikishe kuwa Mifumo ya TEHAMA iko imara na Salama dhidi ya uhalifu wa kimtandao. Uongozi uliwahakikishia wajumbe kuwa iko imara.

MAAZIMIO YA MKUTANO MKUU 2026

Yafuatayo ni Maazimio 10 yaliyotolewa kwenye Mkutano Mkuu wa Wanachama Septemba 19, 2026 Jijini Dodoma

1. Kila Mwanachama aendelee Kuwa Balozi wa kuleta wateja FADEMO.
2. Ofa ya Kwenda Mapumziko Zanziba isogezwa hadi 30.10.2026
3. Wanachama Wawekezaji Wakubwa watapewa ofa ya Ziara nchini RWANDA
4. Kutafuta Wanachama/Wawekezaji Wapya wapatao 1000 kwa mwaka 2027
5. Mwekezaji anaruhusiwa kutoa faida au Uwekezaji baada ya Miezi 3
6. Watendaji wa FADEMO waendelee na Juhudi walizoonesha 2026
7. Kuendelea kuwapa MAFUNZO kuwanoa watoa elimu na Masoko
8. Wafanyakazi na Wanachama wawe mfano wa Uwekezaji Fademo
9. Mfuko unavyokua, Mpango wa Bima ya Afya kwa wanachama uanze.
10. Mkutano Mkuu wa Kufunga Mwaka 2026 huenda ukafanyikia Jijini Mwanza. Lakini itategemeana na hali ya hewa (el-nino) na uwezo wa kifedha.

Tangazo la Ofa ya Ziara

RWANDA VISIT 2027 OFFER

WANACHAMA WA FADEMO WATATEMBELEA RWANDA MWAKA 2027 KWA UDHAMINI WA OFISI, ENDAPO TU MASHARTI YAFUATAYO YATAZINGATIWA.

1. Wekeza angalau TZS 2,000,000 Wewe Mwenyewe

2. Au shawishi Wawekezaji 10 Wawekeze 1,000,000

3. Au wawekezaji 20 wanaowekeza TZS 500,000 kila mmoja.

MWISHO WA OFA NI 30 OCTOBER 2027

Safari inatarajiwa kuwa Mwezi Disemba 2027